**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## MKUTANO WA TANO

## KIKAO CHA PILI

**02 NOVEMBA, 2016**

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

---

## MKUTANO WA TANO

## KIKAO CHA PILI – TAREHE 02 NOVEMBA, 2016

**I. DUA:**

**II. MASWALI:**

**OFISI YA WAZIRI MKUU:**

**16. MHESHIMIWA EZEKIEL MAGOLYO MAIGE (MSALALA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu:- Kutokana na mabadiliko ya tabia nchi matukio ya majanga na maafa kama mvua za mawe pamoja na matetemeko ya ardhi yameanza kutokea mara kwa mara na mara zote Serikali imekuwa haina maandalizi ya kifedha na vifaa kusaidia wahanga kwa muda mfupi na muda mrefu na badala yake imekuwa ikitegemea zaidi wasamaria wema wa mataifa mengine:-

(a) Je, ni kwa nini Serikali imekuwa haisaidii kifedha na vifaa zaidi ya kuhamasisha wasamaria wema wasaidie na wenyewe kubaki na jukumu la kupeleka wataalam kama madaktari na kuratibu misaada pekee;

(b) Je, ni kwa nini Serikali isianzishe mfuko wa maafa kitaifa ambao utakuwa unachangiwa wakati wote kwa njia endelevu.

## OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

**17. MHESHIMIWA JUMAA HAMIDU AWESO (PANGANI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):- Hospitali ya Wilaya ya Pangani ina uhitaji wa X-ray ili kutoa huduma hiyo kwa wananchi ambao hutembea mwendo mrefu kufuata huduma hiyo Tanga Mjini:-

Je, ni lini Serikali itapeleka X-ray katika Hospitali hiyo.

**18. MHESHIMIWA JASSON SAMSON RWEIKIZA (BUKOBA VIJIJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):- Bukoba Vijijini kuna Shule za Sekondari za Serikali na za Wananchi zipatazo 29 ambazo zinaishia Kidato cha 4 na moja kati ya hizo ina Kidato cha 5 na 6 hali inayosababisha wahitimu wengi wanamaliza Kidato cha 4 wakiwa na sifa za kuingia Kidato cha 5 kukosa nafasi:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga madarasa na miundombinu inayofaa kwa Kidato cha 5 na 6 kwenye baadhi ya shule zilizopo ili kutatua tatizo hilo.

**WIZARA YA MAJI NA UMWAGILIAJI:**

**19. MHESHIMIWA GOODLUCK ASAPH MLINGA (ULANGA)**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji:- Mradi wa maji wa umwagiliaji Lupiro umesimama na haijulikani ni lini utaendelea kujengwa:-

Je, ni lini Serikali itatoa fedha kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa mradi huo.

**WIZARA YA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:**

**20. MHESHIMIWA MACHANO OTHMAN SAID (BLW):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki:- Serikali yetu kwa muda imekuwa na uhusiano wa karibu na watu wa China na Serikali ya watu wa China ina Ubalozi Dar es Salaam na Ubalozi mdogo huko Zanzibar:-

(a) Je, Serikali haioni kuwa sasa umefika wakati wa kufungua Ubalozi mdogo wa Tanzania katika Mji wa Guang-Zhou ili kutoa huduma nzuri kwa Watanzania wengi katika Mji huo;

(b) Je, ni utaratibu gani unatumika katika kuwapatia Visa Watanzania ambao wameamua kuishi China kwa zaidi ya mwaka mmoja.

**WIZARA YA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:**

**21. MHESHIMIWA SAVELINA SILVANUS MWIJAGE (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi:- Mkoa wa Kagera una mabonde mengi ambayo yanaweza kuzalisha vyakula pamoja na mboga mboga hususan mabonde ya Kalebe, Kagera, Kyabakoba:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuyaendeleza mabonde hayo ili Vijana waweze kupata ajira;

(b) Je, ni lini Serikali itawapa mikopo Wanawake na Vijana ili waweze kujiongezea kipato.

## WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

**22. MHESHIMIWA FAKHARIA SHOMAR KHAMIS (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:- Kwa muda mrefu sasa kumekuwa na matukio ya kuvamiwa kwa Askari wetu wakiwa katika vituo vyao vya kazi na kujeruhiwa, kunyang'anywa silaha na wakati mwingine hata kuuawa:-

(a) Je, Serikali inatoa tamko gani juu ya usalama wa Askari hawa;

(b) Je, mpaka sasa Serikali imeshakamata silaha ngapi zilizoporwa kutoka kwa Askari waliovamiwa wakiwa katika majukumu yao.

**23. MHESHIMIWA HAWA SUBIRA MWAIFUNGA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:- Mkoa wa Tabora unakabiliwa na tatizo kubwa la msongamano wa mahabusu kiasi cha kutishia afya zao kwa sababu Magereza hayo yana uwezo wa kuchukua takribani Mahabusu 1200 lakini mpaka sasa kuna zaidi ya Mahabusu 2500 kinyume kabisa na haki za Mahabusu:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kuwa hali za Magereza katika Mkoa wa Tabora zinaboreshwa na idadi hiyo ya Mahabusu inazingatia haki za msingi za binadamu;

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kesi zilizopo Mahakamani zinaharakishwa kwa kuwa wapo Mahabusu wengi ambao wana kesi za kubambikiwa au kughushiwa tu.

**WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:**

**24. MHESHIMIWA PASCAL YOHANA HAONGA (MBOZI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi:- Katika Kijiji cha Isenzanya Wilayani Mbozi, shamba lenye ukubwa wa hekari 1000 linalohodhiwa na Mzungu aitwaye Joseph Meya halijaendelezwa kwa miaka mingi sasa huku Wananchi wa Kijiji hicho wakiwa hawana maeneo ya kilimo:-

Je, Serikali haioni ni wakati muafaka wa kulirejesha shamba hilo kwa Wananchi.

## WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:

### 25. MHESHIMIWA PETER AMBROSE LIJUALIKALI (KILOMBERO):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano:- Tangu awamu zilizopita hadi Serikali ya Awamu ya Tano Wananchi wa Kilombero wamekuwa wanapewa ahadi za ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami kutoka Kidatu hadi Ifakara na kutoka Ifakara hadi Mlimba:-

(a) Je, Serikali haitambui mchango wa Wilaya ya Kilombero katika Nchi wa kulisha Taifa;

(b) Kitendo cha Serikali ya Awamu hii kuahidi ujenzi wa viwanda wakati eneo muhimu kwa uchumi wa nchi kama Kilombero likiachwa bila barabara inayosafirisha wakulima na mazao; Je, maana yake ni nini.

### 26. MHESHIMIWA JEROME DISMAS BWANAUSI (LULINDI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano:- Serikali kupitia Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano ililihakikishia Bunge kuwa madaraja ya Mto Mresi katika barabara ya Ulinzi na Shaurimoyo na Nachalolo katika Mto Mwiti yalizolewa na mafuriko na yatajengwa kwa dharura:-

(a) Je, ni maandalizi gani yamefanyika ili madaraja hayo yajengwe kwa haraka;

(b) Je, madaraja hayo yataanza kujengwa lini.

**27. MHESHIMIWA DKT. CHRISTINE GABRIEL ISHENGOMA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano:-

Je, ni nini Mkakati wa Serikali wa kuanza ujenzi wa daraja la Kilombero na utakamilika lini na kuanza kutumika.

**WIZARA YA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:**

**28. MHESHIMIWA VEDASTO EDGAR NGOMBALE (KILWA KASKAZINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa:- Tanzania ni moja ya nchi duniani zilizoathirika kutokana na Tawala za Kikoloni na Vita ya Majimaji ni moja ya vielelezo vya athari hizo ambapo vita hivyo vilianzia Wilayani Kilwa katika Kijiji cha Nandete Mwaka 1905 - 1907:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha waathirika wa vita vya majimaji wanapata fidia kutoka kwa utawala wa kikoloni wa Kijerumani.

**WIZARA YA NISHATI NA MADINI:**

**29. MHESHIMIWA OMARY MOHAMED KIGUA (KILINDI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini:- Serikali kupitia Wizara ya Nishati na Madini kwa kutambua umuhimu wa wachimbaji wadogo wadogo imekuwa ikitoa ruzuku ili kuwawezesha wachimbaji kunufaika na madini yapatikanayo katika maeneo mbalimbali nchini:-

(a) Je, mpango huo umenufaisha wachimbaji wangapi nchini;

(b) Je, ni Mikoa na Wilaya zipi zilizonufaika na mpango huo;

(c) Je, Serikali ipo tayari kuweka utaratibu wa kuwakopesha wachimbaji wadogo wadogo ili kuwawezesha kuchimba madini.

**30. MHESHIMIWA JESCA DAVID KISHOA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini:-

Kwa muda mrefu kumekuwa na habari za uamuzi wa Serikali wa kushirikiana na wadau wa maendeleo kujenga kituo cha kuzalisha umeme wa upepo katika Mkoa wa Singida:-

Je, ni lini mradi huo utatekelezwa.

## III. HOJA ZA SERIKALI:

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:**

Kwamba, Bunge lipokee, kujadili na kushauri kuhusu Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa unaokusudiwa kutekelezwa na Serikali pamoja na Mwongozo wa Kuandaa Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha, 2017/2018.

***(Majadiliano yanaendelea)***

**DODOMA** **DKT. T. D. KASHILILAH**
**02 NOVEMBA, 2016** **KATIBU WA BUNGE**

PARLIAMENT OF TANZANIA • BUNGE LA TANZANIA • UHURU NA UMOJA